JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

UAMUZI WA MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO (MB) WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII KUHUSU MAPITIO YA UAMUZI WA WAZIRI KUFUTA UMILIKI WA KITALU CHA UWINDAJI CHA *LAKE NATRON GAME CONTROLLED AREA EAST* KUTOKA KWA KAMPUNI YA UWINDAJI YA *GREEN MILE SAFARIS LIMITED*

29 APRILI, 2021

YAHUSU: **MAOMBI YALIYOLETWA NA KAMPUNI YA *GREEN MILES SAFARIS* DHIDI YA UAMUZI WA MHE. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**

NA

YAHUSU**: UAMUZI WA MAOMBI YA MAPITIO YA KIUTAWALA DHIDI YA MAAMUZI YA WAZIRI WA MALIALISI NA UTALII WA TAREHE 7 AGOSTI, 2019 KWA MUJIBU WA KIFUNGU CHA 38 CHA SHERIA YA WANYAMAPORI NA. 5 YA MWAKA 2009.**

HIVYO BASI INAAMULIWA KWAMBA:

UAMUZI

Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb)

WMU

Chimbuko la mapitio haya dhidi ya Uamuzi wa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, (ambaye katika uamuzi huu atajulikana kama Mheshimiwa Waziri) ni Maombi yaliyoletwa na kampuni ya GREEN MILES SAFARIS LIMITED ambayo katika maamuzi haya itaitwa "*Muomba Mapitio".* Waziri wa Maliasili na Utalii kwa barua yake yenye Kumb. Na. *CBA.177/389/01/281* ya tarehe 7 Agosti 2019 alifuta umiliki wa *Muomba Mapitio"* wa kitalu cha Lake Natron Game Controlled Area-East. *Muomba Mapitio"* kupitia mwanasheria wake *(Law Associates Advocates)* alimwandikia Waziri barua yenye Kumb. Na. *GMS/0571.19.002.Let2,* ya tarehe 9 Agosti, 2019 akionesha kutokubaliana na uamuzi wa Mheshimiwa Waziri na akiomba mapitio ya uamuzi huo. Maombi hayo ya Mapitio ya Kiutawala (Administrative Review) yalifanyika kwa mujibu wa kifungu cha 38 (14) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, ambacho kinamtaka mtu yeyote asiyeridhika na uamuzi wa Mheshimiwa Waziri wa kufuta umiliki kitalu cha uwindaji kuomba marejeo ya kiutawala kwa Mheshimiwa Waziri husika.

Muomba Maombi anamwomba Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kupitia upya uamuzi wa kufuta umiliki wa kitalu *(Administrative Review)* kama kifungu cha 38(14) kinavyoelekeza na ametoa hoja sita kushajihisha na kumshawishi Mheshimiwa Waziri ili arejeshe umiliki wa Kitalu hicho cha uwindaji kwa Muomba Mapitio. Hoja hizo sita ni:

i. Barua ya Waziri Kumb. Na. *CBA.177/389/01/281* ya tarehe 7 Agosti 2019 haikuainisha sababu za kufuta umiliki wa kitalu cha Lake Natron GCA-East kama kifungu cha 38(12) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009, kinavyoelekeza;

ii. Barua hiyo tajwa ya kufuta umiliki wa Kitalu cha uwindaji cha Muomba Mapitio haikuelezea kosa lolote ambalo Muomba Mapitio amelitenda kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 38 (12) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009.

iii. Muomba Mapitio hakupewa nafasi ya kusikilizwa kama kifungu cha 38(13) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 kinavyoelekeza hivyo maamuzi ya Waziri yamekwenda kinyume na misingi ya haki za asili. (principles of natural justice);

iv. Muomba Mapitio amefanya uwekezaji wa ujenzi mkubwa katika kitalu husika kwa kujenga loji na Kambi ya malazi ya Nyota Tano na kujenga miundombinu ya Maji, Barabara na Umeme katika eneo la kitalu;

v. Muomba Mapitio amefutiwa umiliki wa kitalu katikati ya msimu wa uwindaji wa kitalii na tayari alikuwa na miadi na wageni hadi tarehe 31 Disemba 2019. Aidha, wakati huo baadhi ya wageni walikuwa katikati ya safari za kuwinda hivyo kufuta umiliki wa kitalu si kwamba umeleta hasara na usumbufu kwa wageni bali hasara kwa Serikali pia; na

vi. Kufuta umiliki katikati ya msimu wa uwindaji unaharibu sifa ya Tanzania kama mahali salama pa kufanya uwindaji na inazorotesha juhudi za serikali za kuendeleza utalii.

Pamoja na sababu hizo sita hapo juu Muomba mapitio iliomba kuruhusiwa kuendelea kuwinda mpaka tarehe 31 Disemba, 2019 wakati ombi la kufanyika kwa mapitio ya uamuzi wa kufutiwa umiliki likifanyiwa kazi sababu za maombi hayo ya muda ni kama ifuatavyo:

a. Muomba Mapitio alikuwa ameshapokea fedha kutoka kwa wageni katika kipindi chote cha msimu wa uwindaji wa kitalii wa mwaka 2019;

b. Wakati uamuzi wa kufuta umiliki ukitolewa, tayari Muomba Mapitio alikuwa na wageni wakiwa porini wanawinda;

c. Baadhi ya wageni walikuwa wameshalipa Serikalini ada za vibali vya kuwinda na ada za wageni watazamaji; na

d. Kukatisha safari za wageni ambao wako porini wanawinda kutaleta usumbufu na kuharibu taswira ya nchi katika tasnia ya uwindaji wa kitalii.

Maombi hayo hapo juu (a) – (d) kwa pamoja yalikubaliwa hivyo Muomba Mapitio aliruhusiwa kuendelea na shughuli za Utalii wa uwindaji mpaka Disemba 31, 2019 ambapo maamuzi ya kufuta kibali / leseni / umiliki wa kitalu husika ulianza kuwa na nguvu za kisheria kwa mujibu wa uamuzi wa Mheshimiwa Waziri.

Maombi ya Mapitio ambayo yaliwasilishwa tarehe 9 Agosti, 2019 hayakusikilizwa mpaka tarehe 6 Novemba, 2020 ambapo Muomba Mapitio aliandika tena barua Kumb. Na. *03/01/20* kukumbushia kufanyika kwa mapitio ya maombi yake ya kurejeshewa Kitalu cha Uwindaji cha Lake Natron – East (*Admimistrative review)*.

Tarehe 8 Februari, 2021, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb) alimwandikia Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii *(Hunting Block Allocation Advisory Committee – HBAAC) ambayo katika uamuzi huu itaitwa **"Kamati"*.** Barua hiyo Kumbukumbu Na. CBA.177/389/01/12 iliandikwa kwa mujibu wa kifungu cha 38 (15) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009, ambacho kinamtaka Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuwasilisha maombi ya mapitio kwa Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii *(Hunting Block*

Allocation Advisory Committee – HBAAC) kwa maoni na ushauri. Barua hiyo ilikuwa na hadidu za rejea zifuatazo: -

i. Kufanya mapitio ya Maombi ya Muomba mapitio ya kufutiwa umiliki wa kitalu cha uwindaji cha Lake Natron GCA East kwa mujibu wa Kifungu 38(15) cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009;

ii. Katika kushughulikia suala hili, hakikisha unakutana na kufanya mahojiano na wadau muhimu ikiwemo Muomba Mapitio, Wengert Windrose Safaris na wengine kadri utakavyoona inafaa ili taarifa yako inisaidie kutoa maamuzi.

Tarehe 15 Machi, 2021, Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii *(Hunting Block Allocation Advisory Committee – HBAAC),* iliwasilisha maoni na mapendekezo yao kwa mujibu wa Kifungu 38(15) cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009.

Sasa baada ya kujiridhisha juu ya Mamlaka niliyonayo kisheria na kupata maoni na mapendezo ya Kamati ya Ushauri wa Ugawaji wa Vitalu vya Uwindaji wa Kitalii *(Hunting Block Allocation Advisory Committee – HBAAC),* kwa mujibu wa vifungu vya 38 (14), (15) na (16) vya Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, Pamoja na kanuni zake, ninaanza kushughulikia suala hili.

Kwa faida ya Watanzania na wote watakaopenda kufuatilia mgogoro huu na uamuzi wake ni vema kuongelea historia ya Pori Tengefu la Ziwa Natron pamoja na chimbuko la mgogoro mzima. Pori Tengefu la Lake Natron (Lake Natron Game Controlled Area – LNGCA) ni moja ya maeneo yanayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA). Pori hilo lilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Namba 269 la mwaka 1974 na lina ukubwa wa kilomita za mraba 7,913. Pori hili lipo katika Wilaya za Longido na Ngorongoro Mkoani

Arusha. Kwa upande wa kaskazini linapakana na nchi ya Kenya. Kutokana na umuhimu wa kimataifa wa Pori Tengefu la Lake Natron ki-uhifadhi, mnamo tarehe 4 Julai, 2001, Serikali ya Tanzania ilitangaza pori hilo kuwa eneo la ardhi oevu lenye umuhimu kimataifa chini ya mkataba wa "*Ramsar*".

Kutokana na mgawanyo wa umiliki wa vitalu uliofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii mwaka 2011, ilibainika kuwa majina ya vitalu vya Lake Natron GCA hayakuzingatia uhalisia wa ki-jiografia. Kufuatia hali hiyo, Wizara ilibadilisha majina ya vitalu hivyo ili kuendana na jiografia ya vitalu hivyo bila kubadili mipaka au daraja la kitalu kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo chini:

Jedwali: Majina mapya ya Vitalu vya uwindaji Lake Natron GCA

Na	**Jina la Kitalu la Awali**	**Jina Jipya**
1	Lake Natron GCA (North-South)	Lake Natron GCA (North)
2	Lake Natron GCA (North)	Lake Natron GCA (East)
3	Lake Natron GCA (South-West)	Lake Natron GCA (West)
4	Lake Natron GCA (South)	Lake Natron GCA (South)

Baada ya zoezi la nchi nzima la kutathimini ukubwa wa vitalu lililofanyika mwaka 2009, Pori Tengefu la Lake Natron ambalo awali lilikuwa na vitalu viwili liligawanywa katika vitalu vinne. Vitalu hivyo pamoja na kampuni zilizomilikishwa katika ugawaji wa mwaka 2011 kwa kipindi cha umiliki cha 2013-2018 ni: *Lake Natron Game Controlled Area (GCA) North (iliyomilikishwa kwa Wengert Windrose Safaris - WWS), Lake Natron South (iliyomilikishwa kwa Kilombero North Safaris - KNS), Lake Natron East (iliyomilikishwa kwa Green Mile Safaris Ltd – GMSL ambaye ni muomba mapitio) na Lake Natron West (iliyomilikishwa kwa Michel Mantheakis Safaris Ltd-MMSL)*

Baada ya kugawanywa na kukamilisha umilikishwaji wa vitalu vya Lake Natron GCA mwaka 2011, Kampuni ya Wengert Windrose Safaris haikuafiki uamuzi uliofanywa na Serikali wa kuimilikisha Green Mile Safaris Limited kitalu cha Lake Natron Game Controlled Area – East. Kampuni ya Wengert Windrose Safaris iliingia katika mgogoro na Serikali kuhusu umiliki wa kitalu hiki. Sababu kubwa ya kung'ang'ania kitalu hicho ni uwekezaji wa miundombinu iliyofanya katika kitalu hicho. Aidha, kampuni ya Wengert Windrose Safaris iliituhumu Idara ya Wanyamapori kuwa haikubadilisha majina ya vitalu tu bali ilifanya *"swapping"* ya vitalu hivyo.

Kufuatia hali hiyo, kampuni ya Wengert Windrose Safaris ilimuomba Waziri mwenye dhamana, kufanya mapitio (*administrative review*) ya ugawaji wa vitalu vya Lake Natron Game Controlled Area kwa mujibu ya Kifungu cha 38(14) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009.

Mapitio ya maombi ya Wengert Windrose Safaris yalibaini kuwa Wizara ilibadilisha majina ya vitalu vya Lake Natron Game Controlled Area bila kuathiri mipaka na madaraja husika. Kwa msingi huo, maombi ya Wengert Windrose Safaris, yalikataliwa. Kufuatia hali hiyo, kampuni ya Wengert Windrose Safaris ilifungua kesi mbalimbali katika Mahakama Kuu, Mahakama ya Ardhi na Mahakama ya biashara kupinga uamuzi wa Serikali kwa kuishitaki Serikali na wadau wengine.

Pamoja na kesi zilizofunguliwa, mwaka 2013 Wengert Windrose Safaris iliishitaki Serikali ya Tanzania kwenye Bunge la Congress nchini Marekani ikiituhumu Idara ya Wanyamapori kubadili majina ya vitalu na kugawa kitalu kilichokuwa kinamilikiwa na kampuni hiyo kwa kampuni ya Green Mile Safaris Limited. Wabunge wa Congress walimwandikia Rais wa Marekani Mhe. Barack Obama wakimtaka kuongelea suala hilo katika ziara yake nchini Tanzania.

Serikali ilitoa ufafanuzi na kukanusha tuhuma hizo kwa kuwa vitalu viligawanywa kwa mujibu wa sheria na hapakuwepo na kampuni iliyopendelewa. Vilevile, taarifa zinaonesha kuwa Wengert Windrose Safaris ilishindwa katika kesi ilizokuwa imefungua dhidi ya Serikali. Hata baada ya kushindwa kesi, kampuni ya Wengert Windrose Safaris iliendelea kutumia mbinu mbalimbali za kutaka kupata kitalu cha Lake Natron Game Controlled Area – East bila mafanikio.

Tarehe 07 Agosti, 2019 aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt. Hamisi A. Kigwangalla (Mb), kwa kutumia mamlaka yake chini ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Sura ya 283 alimfutia Muomba Mapitio umiliki wa kitalu cha Lake Natron Game Controlled Area - East kwa barua yake yenye Kumb. Na. *CBA.177/389/01/281.*

Tarehe 09 Agosti, 2019 Wizara ilitoa maelekezo mahususi kwa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) kuhusu utekelezaji wa uamuzi wa kufuta umiliki wa kitalu. Maelekezo hayo yalilenga kuondoa usumbufu kwa wageni ambao walikuwa porini wakiwinda na kulinda heshima ya Tanzania katika tasnia ya uwindaji wa kitalii. Maelekezo hayo ni:-

a) Kumpatia Muomba Mapitio muda wa kumalizana na wageni wake ambao walikuwa wamelipa kwa ajili ya kuja kufanya uwindaji wa kitalii;
b) Wilaya ya Longido ielekezwe kutoingilia kwa pupa utekelezaji wa namna ya kumuondoa au kuondoka kwa mwekezaji. Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Longido alielekezwa kusitisha maagizo aliyoyatoa ya kuzuia mali, kufukuza wageni na kukamata watumishi wa Muomba Mapitio; na
c) Kuimarisha ulinzi wa kitalu katika kipindi cha mpito na mali za Muomba Mapitio zisihujumiwe kwa makusudi.

Mbele ya meza yangu kuna maombi ya mapitio ambayo yameletwa na muomba mapitio kupitia kampuni uwakili ya Law Associates. Katika Maombi hayo kuna hoja sita za kisheria ambazo ninawajibika kuzitolea uamuzi ama moja moja; ama kwa ujumla wake. Hoja hizo, ambazo nimezijadili hapo awali, nazinukuu hapa chini kwa urahisi wa rejea: Hoja hizo ni:

i. Barua ya Waziri Kumb. Na. *CBA.177/389/01/281* ya tarehe 7 Agosti 2019 haikuainisha sababu za kufuta umiliki wa kitalu cha Lake Natron GCA-East kama kifungu cha 38(12) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009, kinavyoelekeza;

ii. Barua hiyo tajwa ya kufuta umiliki wa Kitalu cha uwindaji cha Muomba Mapitio haikuelezea kosa lolote ambalo Muomba Mapitio amelitenda kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 38 (12) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009.

iii. Muomba Mapitio hakupewa nafasi ya kusikilizwa kama kifungu cha 38(13) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 kinavyoelekeza hivyo maamuzi ya Mheshimiwa Waziri yamekwenda kinyume na misingi ya haki za asili. (principles of natural justice);

iv. Muomba Mapitio amefanya uwekezaji wa ujenzi mkubwa katika kitalu husika kwa kujenga Loji na Kambi ya “Nyota Tano” na kujenga miundombinu ya Maji, Barabara na Umeme katika eneo la kitalu;

v. Muomba Mapitio amefutiwa umiliki wa kitalu katikati ya msimu wa uwindaji wa kitalii na tayari ilikuwa na miadi na wageni hadi tarehe 31 Disemba, 2019. Aidha, wakati huo baadhi ya wageni walikuwa katikati ya safari za kuwinda hivyo kufuta umiliki wa kitalu si kwamba umeleta hasara na usumbufu kwa wageni bali hasara kwa Serikali pia; na

vi. Kufuta umiliki katikati ya msimu wa uwindaji unaharibu sifa ya Tanzania kama mahali salama pa kufanya uwindaji na inazorotesha juhudi za Serikali za kuendeleza utalii.

Kwa tathmini yangu ya haraka, nimezigawa hoja hizo sita hapo juu katika makundi makubwa mawili. Hoja i, ii na iii ni hoja za kisheria na hoja iv, v na vi ni hoja za kiuchumi. Kwa muktadha huo ninajielekeza kujibu kwanza hoja za kisheria kabla sijaenda kwenye zile za kiuchumi.

Katika hoja namba moja na namba mbili, ambazo ningependa kuzijadili kwa pamoja kutokana na kushabiiana na kuwa na mzizi katika kifungu kimoja cha sheria, Muomba Mapitio anakosoa uamuzi wa Mheshimiwa Waziri akielezea kuwa "Barua ya Mheshimiwa Waziri Kumb. Na. *CBA.177/389/01/281* ya tarehe 7 Agosti, 2019 haikuainisha sababu za kufuta umiliki wa kitalu cha Lake Natron GCA-East kama kifungu cha 38(12) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009, kinavyoelekeza". Pia anaendelea kueleza kuwa "Barua hiyo tajwa ya kufuta umiliki wa Kitalu cha uwindaji cha Muomba Mapitio haikuelezea kosa lolote ambalo Muomba Mapitio amelitenda kama ilivyobainishwa katika kifungu cha 38 (12) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009".

Hoja hizi Mbili pacha zinatokana na Kifungu cha 38(12) cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Sura 283, ambacho kinasomeka;

> *"Notwithstanding the provisions of this section, the Minister may, at any time before the expiration of the period of a hunting term, cancel the allocation of a hunting block, where, there is sufficient evidence that the person allocated a hunting block: -*

(a) has failed to satisfy any or a combination of matters required by the Minister to take into consideration;

(b) gave false or incorrect information on the application for a hunting block;

(c) has been convicted of an offence under this Act;

(d) has failed to pay the necessary fees or any other debt due to him in relation to his hunting block; or

(e) has sublet a hunting block allocated to him"

Katika hoja za Muomba mapitio amedai kuwa Mheshimiwa Waziri amekiuka kifungu hicho na katika Ushahidi wake alioutoa tarehe **29 Machi, 2021** mbele yangu alirejea hoja hiyo. Barua ya Mheshimiwa Waziri *CBA.177/389/01/281* ya tarehe 7 Agosti, 2019, iliyoandikwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Muomba Mapitio, inatamka kuwa:

"I, Dr. Hamis A. Kigwangala, Minister for Natural Resources and Tourism, by virtue of powers conferred upon me by section 38 of the Wildlife Coservation Act No. 5 of 2009 do hereby cancel the allocation of the hunting block Lake Natron East with effect from 7th day of August, 2019".

Mbele yangu sina Ushahidi unaonesha kuwa kabla ya kufutiwa umilikiwa kitalu cha uwindaji Muomba Mapitio alijulishwa kosa lake na kupewa sababu za uamuzi kama ambavyo kifungu cha sheria kinataka. Barua ya Mheshimiwa Waziri hapo juu inaelezea mamlaka yake katika kufuta umiliki wa Kitalu lakini hailezei kosa ambalo Muomba Mapitio amelitenda kiasi cha kustahili matumizi ya mamlaka ya Mheshimiwa Waziri na adhabu aliyopewa.

Hata hivyo, barua ya Waziri haikuonesha; vifungu vya sheria vilivyokiukwa. Kutokana na Ushahidi wa Muomba Mapitio, barua ya Mheshimiwa Waziri na maoni na ushauri wa kamati ya Ushauri iliyotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 38 (15) na (16) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009, hakuna shaka kuwa uamuzi wa Mheshimiwa Waziri alioutoa tarehe 7 Agosti, 2019 kupitia barua Kumb. Na. *CBA.177/389/01/281,* unakinzana na kifungu cha 38(12) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 ambacho kinataka sababu iwekwe bayana. Hivyo basi hoja hii ya Muomba Mapitio ina mashiko kwa misingi kuwa sio tu muomba mapitio hakuelezwa sababu ya uamuzi, bali pia hakuelezwa kosa lake. Kwasababu hiyo, hoja namba moja na mbili zinaamuliwa kwa manufaa ya muomba mapitio.

Muomba Mapitio, katika hoja yake ya tatu anadai kuwa "Muomba Mapitio hakupewa nafasi ya kusikilizwa kama kifungu cha 38(13) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 kinavyoelekeza; hivyo maamuzi ya Waziri yamekwenda kinyume na misingi ya haki za asili *(principles of natural justice)*. Kifungu cha 38(13) cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Sura ya 283 kinasomeka;

> *"No decision to cancel the allocation of a hunting block shall be made until the person concerned has been given an opportunity to be heard"*

Haki ya kusikilizwa inamaanisha fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu na kwa haki. Haki hii inajumuisha kupewa taarifa ya kutosha na ya mapema ya kesi ili kupata muda wa kuandaa majibu ya kesi dhidi yake, kupewa nafasi ya kutoa ushahidi wake kwa ukamilifu (ikiwani pamoja na kuita mashahidi), kupewa fursa ya kuwauliza maswali washitaki wake na kupewa fursa ya kuwakilishwa, kama ilivyoelezwa kwenye Ibara ya 13 (6) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano waTanzania. Ibara hiyo inatamka;

"13 (6) Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, Mamlaka ya Nchi itaweka taratibu zinazofaa au zinazozingatia misingi kwamba -

(a) wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahakama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu, na pia haki ya kukata rufaa au kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo hicho kingenecho kinachohusika";

Katika kesi ya **Ridge V. Baldwin (1963) 1.Q.B.539,** Mahakama ya Uingereza ilitamka kuwa**;**

" kumnyima mlalamikiwa haki maridhawa ya kusikilizwa kunafanya uamuzi kuwa batili kisheria".

Mahakama ya Tanzania katika kesi ya Mohamed **Kitwana vs Mohamed Mang'uro** kesi ya rufaa Na. 193 ya Mwaka 2004, Jaji Shangwa alitamka kuwa;

" Natamka kuwa Uamuzi wa Hakimu Mkazi Mkuu ni batili kwa kutompa mkata rufaa fursa maridhawa ya kuwasilisha kesi yake".

Muomba Mapitio hakupewa mashitaka dhidi yake wala nafasi ya kujitetea kabla ya kufutiwa leseni ya Uwindaji wa kitalii katika kitalu tajwa. Mamlaka ya kiutawala, pale ambapo inatekeleza majukumu ya kimahakama na kuwa na mamlaka ya kuamua jambo kwa kadiri inavyoona inafaa (discretionary powers), inalazimika kufuata misingi kadhaa ikiwemo kuheshimu haki ya kusikikizwa ambayo ni ya asili, lakini pia imeelezwa na ibara ya 13 (6) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977. Muhimu Zaidi katika shauri hili ni kifungu cha 38 (13) cha Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka

2009 ambayo imeeleza bayana kuwa lazima mtu asikilizwe kabla ya kufutiwa kibali cha Kitalu cha uwindaji wa kitalii katika kitalu.

Ushahidi wa Muomba Mapitio ni kuwa hajawahi kusikilizwa kabla ya uamuzi wa tarehe 7 Agosti, 2019 wa kufuta umiliki wa Kitalu cha Lake Natron - East. Barua ya Mheshimiwa Waziri tajwa hapo juu haionyeshi kuwa Muomba Mapitio alipewa fursa ya kusikilizwa kwa maandishi au ana kwa ana au kwa kuita mashahidi. Maoni na Mapendekezo ya Kamati nayo yanaelezea msimamo huo huo. Haki ya kusikilizwa na kujitetea kabla ya kuadhibiwa ni haki ya msingi ambayo lazima izingatiwe na chombo chochote kinachofanya shughuli za kimahakama. Mamlaka ya Mheshimiwa Waziri katika kifungu cha 38 cha sheria ya Wanyamapori ni mamlaka ya kimahakama, hivyo misingi ya haki za asili lazima izingatiwe.

Muhimu zaidi ni matakwa ya kikatiba Ibara 13(6) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 na sheria ya Wanyampori Na. 5 ya Mwaka 2009, hususan katika kifungu 38(13) ambacho kinatamka kuwa maamuzi yoyote yasifanyike mpaka mtu ambaye maamuzi hayo yanamlenga apewe haki ya kusikilizwa. Kutokana na Ushahidi uliopo, ni bayana kuwa Muomba Mapitio hakusikiliwa. Ushahidi wa barua ya Mheshimiwa Waziri Kumb. Na. CBA.177/389/01/281 ya tarehe 7 Agosti, 2019 haisemi kuwa Muomba Mapitio alisikilizwa. Maoni na Mapendekezo ya Kamati nayo yanabainisha kuwa;

> *"uamuzi wa kuifutia GMSL umiliki wa kitalu cha Lake Natron GCA – East haukufuata matakwa ya kisheria na misingi ya utawala bora. Aidha, hatua ya Wizara ya kutoa maelekezo siku mbili baada ya kufutwa kwa umiliki ya kuruhusu Muomba Mapitio kukamilisha safari za wageni inaonesha kuwa maamuzi ya kufuta umiliki hayakuwa na uchambuzi wa kina kabla ya kutolewa".*

Ni ushauri mgumu na mchungu kwa Wizara lakini ninalazimika kuupokea, kuukubali na kuufanya sehemu ya Uamuzi wangu katika suala hili kwasababu ndio ukweli kwa mujibu wa Ushahidi uliopo mbele yangu. Hivyo basi hoja ya tatu ya Muomba Mapitio kuwa hakupewa fursa ya kusikilizwa kabla ya Uamuzi wa kumnyang'anya kitalu cha uwindaji, nayo inaamuliwa kwa manufaa ya Muomba mapitio.

Kuhusu hoja za kiuchumi namba iv, v na vi, sina sababu tena ya kuendelea kuzijadili kwasababu; mosi zinataka Ushahidi wa kina, na Pili mjadala wake ni sawa na zoezi la kitaaluma kutokana na ukweli kuwa hoja za kisheria zimemaliza, kwa kiasi chote, misingi ya uamuzi huu. Pia uamuzi wa Wizara kumruhusu muomba mapitio kufanya uwindaji wa Kitalii mpaka tarehe 31 Disemba, 2021 ulijibu baadhi ya hoja hizo.

Wakati wa kusikiliza mapitio haya, yamejitokeza mambo kadhaa kupitia Ushahidi uliotolewa au ushauri wa Kamati mambo hayo ni:

i. Kuzorota kwa mahusiano kati ya Mkuu wa Wilaya ya Longido na Muomba Mapitio.
ii. Wadau mbalimbali kuhusika kwa namna moja au nyingine katika kuchochea mgogoro wa umiliki wa kitalu cha Lake Natron Game Controlled Area-East.
iii. Kuna mkataba kati ya Wengert Windrose Safaris na Wilaya ya Longido wa ujenzi wa kambi ya utalii katika msitu wa Gelai. Kutokana na mkataba huo, ndio sababu ya kutokuondosha kambi hiyo ambayo hadi sasa ipo wakati eneo hilo ni la Muomba Mapitio.
iv. Uongozi wa Wilaya ya Longido na vijiji vinavyozunguka kitalu cha Lake Natron Game Controlled Area - East kwa kufahamu au kutofahamu

umekuwa sehemu ya mgogoro wa umiliki wa kitalu cha Lake Natron Game Controlled Area – East.

Mambo haya siwezi kuyatolea maamuzi kwasababu sio sehemu ya hoja zilizoletwa kwa Mheshimiwa Waziri kwa barua ya tarehe 07 Agosti, 2019 lakini Wizara itatafuta njia muafaka ya kisheria na kiutawala ya kuyashughulikia.

Kufuatia uchambuzi uliofanyika kuhusu uamuzi wa kufutiwa umiliki wa kitalu cha Lake Natron – East, nimejiridhisha kuwa malalamiko ya Muomba Mapitio Mile Safaris Limited yana msingi wa kisheria, na barua ya Mhe. Waziri ya kufuta umiliki wa kitalu haikuzingatia sheria na misingi ya utawala bora. Hivyo, ninaamua na kuagiza yafuatayo: -

i. Muomba Mapitio arejeshewe umiliki wa kitalu cha Lake Natron Game Contolled Area-East hadi mwaka 2022;
ii. Iandaliwe rasimu “template” itakayotumiwa katika umilikishaji wa vitalu itakayoonesha “terms and conditions” za kufuatwa na mwekezaji wakati wote wa umiliki wa kitalu;
iii. Kuwepo kwa umakini wakati wa kuandika nyaraka za kiofisi, ili kuepusha ukinzani wa sheria na taratibu zilizopo;
iv. Kuweka utaratibu wa kushughulikia migogoro haraka pindi inapojitokeza.
v. Haki ya mwekezaji inaisha pale ukomo wa umiliki unapofika kwa mujibu wa kipindi cha umiliki kilichopo ki-sheria bila kujali kiwango cha uwekezaji alichofanya.
vi. Kama kuna mtu yoyote ana malalamiko ayalete kwa Mheshimiwa Waziri kimaandishi na sio kuleta fujo na taharuki katika jamii.

Maamuzi haya yamezingatia maombi ya mapitio ambayo yaliletwa rasmi na kwa kufuata sheria mbele ya Mheshimiwa Waziri tarehe 7 Agosti, 2019.

Kwa kiasi kikubwa mgogoro huo umezorotesha ustawi wa uhifadhi na biashara, kuchafua taswira ya Tanzania katika tasnia ya uwindaji wa kitalii na kupunguza michango ya maendeleo kwa wananchi. Hivyo, ni vyema Tanzania Wildlife Authority (TAWA) ikahakikisha kuwa sheria, kanuni na miongozo iliyopo imepewa ufumbuzi ili kuepusha matatizo ya namna hii.

Naishukuru Kamati ya ushauri kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kunishauri katika kufikia uamuzi wa suala hili kwa mujibu wa kifungu cha 38(15) cha Sheria ya Wanyamapori Na.5 ya mwaka 2009. Mtu yoyote ambaye hajaridhika na uamuzi huu, ana haki ya kukata rufaa kwa mujibu wa kifungu cha 38(16) cha Sheria ya Wanyamapori Na.5 ya mwaka 2009.

Imetolewa hapa Dodoma leo tarehe 29 Aprili, 2021

……
Dkt. Damas Daniel Ndumbaro (Mb)
Waziri wa Maliasili na Utalii
Dodoma, Tanzania
29 Aprili, 2021